Mwaka wa 1989 kwa ufupi

Ufuat. wa uk.11

vu ya Kaskazini, mlima wa moto Nyamulagira katomboka
23: Maraïs Omar Bongo wa Gabon na Sassou Nguessou wa Kongo kawasili mjini Kinshasa jamhurini Zaïre ambako kakutana katika masimulizi rasmi na Raïs Mobutu kuhusu swali la nchi jirani na rafiki Angola.

MAY:Miaka 22 ya Chama Mapinduzi "MPR"

1:Kumbukumbu la miaka 100 ya sikukuu ya Wafanyakazi ulimwenguni
16: Raïs Mobutu kawasili kiserkali nchini Angola.Mkutano wa kilele kati ya maraïs Dos Santos wa Angola na wenzie wa nchi jirani kuhusu amani nchini Angola. Jamhuri ya Ethiopia kaponyoka mapinduzi ya serkali
20: Chama cha Mapinduzi "MPR" katimiza miaka 22
22: Majimboni mwa Kivu ya Kaskazini na Kusini, uchaguzi kahahirishwa

JUNI:Kamanyola kajipatia sura ya pekee

14: Kardinali Malula, arkiaskofu wa Kinshasa kafariki dunia
19: Sherehe muhimu kafanyishwa mjini Kamanyola (Kivu ya Kusini) kuhusu ukumbusho wa kulazwa kwa wahuni. Maraïs Habyarimana wa Rwanda na Buyoya wa Burundi kashiriki kwa sherehe hizo pembeni ya Mareshali Mobutu bingwa vita hivyo na kuipatia mji wa Kamanyola sura ya pekee siku hiyo.
22: Mkutano wa kilele wa maraïs wa nchi za Afrika ya kati na ya Kusini mjini Gbadolite. Ndugu adui Savimbi Jonas, kiongozi mkuu wa chama UNITA na Eduardo Dos Santos, raïs wa Angola kapezana mkono alama wazi ya kushirikiana siku za usoni kwa maendeleo ya nchi yao Angola.
29: Raïs Mobutu wa Zaïre kapokelewa katika masimulizi rasmi na Bwana Bush, raïs wa Shirikisho la Amerika mjini Washington, mji mkuu wa shirikisho hilo
30: Jamhuri ya Zaïre katimiza miaka 29 tangu hapo kajinyakulia uhuru wake. Serkali ya Sudania kapinduliwa na jemadari Omar Hassan Ahmed El Béchir kawa raïs wa jamhuri

JULAI : Mkutano wa kilele wa umoja wa mataifa huru za Afrika kafanywa

14: Miaka 200 katimia tangu hapo kafanywa mapinduzi nchini Ufaransa
21: Katimia miaka 20 tangu hapo marubani-anga Neil Armstrong na Edwin toka Amerika katembelea mwezi
24-26: Mkutano wa kilele wa Kiumoja wa nchi huru za Afrika kafanywa mjini Addis-Abeba mji mkuu wa Ethiopia na makaa imara ya Umoja huo.Raïs Hosni Moubarak wa Misri kachaguliwa kama vile prezidenti wa umoja na waziri Salim Ahmed Salim kamgomboa bwana Idé Oumarou wa Niger kama vile katibu mkuu wa muungano.

OGUSTI:Bwana Frederik De Klerk kakutana na Raïs Mobutu mjini Goma

8:Wawakilishi wa serkali ya Angola toka Luanda na wa chama UNITA ya daktari Savimbi kakutana katika masimulizi mjini Kinshasa
10: Mwananchi Kalume Mwana Kahambwe, prezidenti wa Bunge la Taifa kafariki nchini Afrika ya Kusini.
19-21: Baba mtakatifu wa Roma, Papa Yoane-Paolo wa Pili katika ziara nchini Hispania
25: Raïs Mobutu wa Zaïre kakutana na bwana Frederik De Klerk katika masimulizi mjini Goma. Katika masimulizi yao swali la mzozo wa Angola kaonywa
26: Mnamo mwaka wa 1973, Umoja wa mataifa kasimika tarehe hiyo kwa ukumbusho wa swali la Namibia. Pia ni siku ya ukumbusho wa haki za mwananchi na za binadamu.

SEPTEMBA:Ndege moja ya shirika UTA kaanguka

12: Watenda maovu, askari kama vile wengineo wananchi, kapelekwa mahakamani mbele ya amzi mjini Kinshasa
15: Bwana Frederik de Klerk kachaguliwa kama vile Raïs wa Jamhuri ya Afrika ya Kusini kwa muda wa miaka mitano. Kamgomboa bwana Pieter Botha
18: Mkutano wa kamati ya pekee kuhusu amani nchini Angola mjini Kinshasa. Maraïs 18 kahuzuria mkutano huo.
19: Ajali kubwa la ndege (gari la mabawa) aina DC 10 la shirika la ufaransa UTA kaanguka katika jangwa la Niger na watu 171 kafariki dunia katika msiba huo.
23-25: Raïs wa Jamhuri ya Tanzania, bwana Ali Hassan Mwinyi na mkewe katika ziara ya kiserkali nchini Zaïre.

OKTOBA : Mwimbaji maalum Luambo Makiadi (Franco) kafariki mjini Namur

1:Ukumbusho wa miaka 50 tangu kuundwa kwa jamhuri ya watu wa China
4:Prezidenti-Muundaji wa Chama cha Mapinduzi "MPR" katoa hotuba ya kusisimua katika mkutano wa 44 wa kawaida wa mkusanyo mkuu wa Muungano wa Umoja wa Mataifa (ONU) nchini Amerika
5-8: Mkutano wa wakristu kuhusu ukaristia mjini Séoul nchini Korea ya Kusini
7:Mwimbaji wa wari na maalum Luambo Makiadi (Franco) kafariki mjini Namur katika Ufalme wa Ubelgigi
14: Mareshali Mobutu katimiza miaka 59 ya kuzaliwa
24: Mapambano ya mwisho (finali) ya Kombe la Zaïre mjini Kinshasa.Timu la Daring Motema Pembe la Kinshasa kaonya lenzie la Mazembe na kuchukua kombe hilo.
27: Sikukuu ya "3Z": Zaïre jito, Zaïre nchi na Zaïre feza.

NOVEMBA: ukuta wa kugawa mji wa Berlin nchini Udachi kabomolewa

9:Ukuta uliokuwa ukigawa Berlin mji mkuu wa Udachi kabomolewa
24: Kagunduliwa kiserkali bwawa (wando) wa moto wa stimu wa Mobayi-Mbongo jimboni Ekwatori
26-29: Bwana Mario Soares, raïs wa Ureno katika ziara ya kiserkali nchini Zaïre.

DESEMBA:Mwaka 1990 katajwa mwaka wa maelimisho

4. Anzuluni Bembe ateuliwa kama kiongozi wa Bunge
6:Jumuia ya Madola (Muungano wa Umoja wa Mataifa) kataja mwaka 1990 kama vile mwaka wa maelimisho
10: Siku ya ukumbusho wa haki za binadamu
17: Bwana Yoakimu Chissano, raïs wa Jamhuri ya Msumbiji katembelea Jamhuri ya Zaïre
18-22: Mkutano wa mawaziri na maliwali wa jimbo kafanywa mjini Kinshasa.

Bisimwa L-B. Tserou

Rugamika na Masu, mali ya M.E.A. imeenda wapi?

Mjini Bukavu, muungano wa masaidiano na uamzi (MEA) katika mkutano wake wa kawaida wa mwaka huu ulioendeshwa mwezi wa Oktoba, ilijulishwa kwa wahuzuriaji kuwa kiasi cha Zaïre 338.100 kiliweza kukusanyishwa ili kuimarisha na kufikilia ukomo wake.

Itakumbushwa wa kamati ya zamani iliyokuwa ikiongozwa na wananchi Rugamika na Masu itashtakiwa utumizi mbaya wa feza za muungano huo. Viongozi hao watezamiwa kupelekwa kwenyi mahakama na waombwa warudishe katika sanduku la muungano kiasi cha zaïre milioni 30 za asili mali na faida kutokana na mikopo iliyowatolea tangu mwaka wa 1984 na mpaka leo hii hairudishwa.

Kamati hiyo mpya yaundwa na wananchi': Bashaga Butabana,(prezidenti) Kabamba wa N'Sibula (Makamu), Chihonzi (katibu), Kasketi (naibu wa katibu), Zigabe (mlinda feza), washauri: Muganzi Mihigo, Shangalume, Biruga, Rukera, Shamavu, Chilangulangu Mufungizi; wachunguzi wa feza: Muchuba, Nabihazire na Masumbuko Kabanja.